JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA MAENDELEO ENDELEVU YA VIWANDA 2025 KWA KIPINDI CHA MWAKA 2025–2035

2025

MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA MAENDELEO ENDELEVU YA VIWANDA 2025 KWA KIPINDI CHA MWAKA 2025–2035

2025

YALIYOMO

YALIYOMO ..... i-ii
VIFUPISHO ..... iv-v
UFAFANUZI WA MANENO vi
1 UTANGULIZI 1
1.1 Umuhimu wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera 1
1.2 Masuala ya Utekelezaji 1
1.3 Majukumu ya Taasisi na Wadau 2
1.4 Matokeo Yanayotarajiwa 2
1.5 Hitimisho 2
2 HALI ILIVYO 3
2.1 Uongezaji wa Thamani na Mnyororo wa Thamani 3
2.2 Viwanda vya Kimkakati 4
2.3 Upatikanaji na Ufikiwaji wa Soko 5
2.4 Utafiti na Ubunifu 6
2.5 Masuala Mtambuka 6
2.5.1 Wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu 6
2.5.2 Uhifadhi wa mazingira 6
2.5.3 VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa 7
3 DIRA, DHAMIRA, NA MALENGO 8
3.1 Dira 8
3.2 Dhamira 8
3.3 Malengo 8
4 MALENGO YA SERA, MIKAKATI, NA SHABAHA 9
4.1 Uongezaji Wa Thamani na Mnyororo wa Thamani 9
4.2 Viwanda vya Kimkakati 10
4.3 Upatikanaji na Ufikiwaji wa Soko 11
4.4 Utafiti na Ubunifu 11
4.5 Masuala Mtambuka 12
5 MFUMO WA KITAASISI 14
6 UTEKELEZAJI WA SERA 17
6.1 Rasilimali Fedha Zinazohitajika 17
6.2 Muda wa Utekelezaji 17
7 UFUATILIAJI NA TATHMINI 28
7.1 Utangulizi 28
7.2 Walengwa 28
7.3 Mipango ya Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini 28
7.3.1 Mpango wa ufuatiliaji 29
7.3.2 Mpango wa mapitio 29
7.3.3 Mpango wa mapitio ya viashiria vya muda mfupi 29
7.3.4 Mpango wa tathmini 29
7.3.5 Mpango wa utoaji taarifa 34
7.4 Ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu 34
7.5 Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini 34
7.5.1 Aina za taarifa za ufuatiliaji na tathmini 34
7.5.2 Ratiba ya utoaji taarifa 35
7.5.3 Mfumo wa utoaji taarifa 35
7.5.4 Mfumo wa kutoa mrejesho 35
7.6 Matumizi ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini 35
7.7 Mpango wa Utekelezaji 35
7.8 Hitimisho 36

ORODHA YA MAJEDWALI
Jedwali Na. 1: Wajibu na Majukumu ya Wadau 14
Jedwali Na. 2: Mpango wa Utekelezaji (2025/26/2035/36) 18
Jedwali 3: Viashiria vya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi 30
Jedwali Na. 4: Ratiba ya Utoaji Taarifa 35

VIFUPISHO

AfCFTA	Eneo Huru la Biashara la Afrika
AZAKI	Asasi za Kiraia
AZISE	Asasi Zisizo za Serikali
CAMARTEC	Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini
DPs	Washirika wa Maendeleo
EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki
EU	Umoja wa Ulaya
FCC	Tume ya Ushindani
KMTC	Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Mitambo cha Kilimanjaro
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa
MCDGWSG	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
MDAs	Wizara, Idara na Wakala
MoE	Wizara ya Nishati
MoEST	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
MoFA	Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki
MoH	Wizara ya Afya
MoIT	Wizara ya Viwanda na Biashara
MoLHHS	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
MoM	Wizara ya Madini
MoNRT	Wizara ya Maliasili na Utalii
MoA	Wizara ya Kilimo
MoF	Wizara ya Fedha
MoHA	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi
MoLF	Wizara ya Mifugo na Uvuvi
MoT	Wizara ya Uchukuzi
MoW	Wizara ya Ujenzi
MoW	Wizara ya Maji
NFRA	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula
PMO	Ofisi ya Waziri Mkuu
PO-PI	Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji
PO-RALG	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
RSs	Sekretarieti za Mikoa
SADC	Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

VIFUPISHO

SIDO	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo
TEMDO	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania
TIRDO	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VPO	Ofisi ya Makamu wa Rais
VVU	Virusi vya UKIMWI
WTO	Shirika la Biashara Duniani

UFAFANUZI WA MANENO

NENO	UFAFANUZI
Kiwanda (wingi viwanda)	Mahali panapofanyika shughuli za uchakataji, utengenezaji ama uunganishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuziuza
Maendeleo ya viwanda	Mafanikio ya ukuaji wa kiuchumi yanayotokana na utafiti, uundaji, majaribio ya tafiti, usambazaji wa teknolojia, mafunzo, ujenzi na uendelezaji wa viwanda
Mazingira wezeshi ya viwanda	Jitihada mbalimbali zinazofanyika ili kuchochea maendeleo ya viwanda
Uendelezaji wa viwanda	Shughuli zinazojumuisha kutafiti, kusanifu, kuanzisha, kuzalisha bidhaa kiwandani, kupima, kuuza, kuendeleza huduma baada ya mauzo, na kuimarisha ubora wa bidhaa kwa lengo la kukuza ushindani.
Ukuaji wa viwanda	Mchakato wa kuhama kutoka katika uchumi unaotegemea kilimo na uzalishaji wa mikono kwenda katika uzalishaji unaotegemea mashine, kupitia utafiti na ubunifu, usanifu, uendelezaji, utengenezaji, upimaji, uzingatiaji wa ubora, mauzo, na huduma za baada ya mauzo, kwa lengo la kuwa mshindani thabiti katika soko la bidhaa husika
Mitaji	Inahusisha miundombinu wezeshi iliyopo, fedha taslimu, malighafi, wataalam, na teknolojia inayohitajika kwa ajili ya uzalishaji kiwandani
Uzalishaji kiwandani	Mchakato wa kubadilisha malighafi mbalimbali kuwa bidhaa katika mazingira ya viwanda; au huduma ili kuongeza thamani.
Uzalishaji wa bidhaa	Sehemu ya uzalishaji kiwandani ambayo huhusisha mchakato wa kubadilisha malighafi kuwa bidhaa kamili zinazoonekana, kwa kutumia hasa mitambo na nguvukazi katika kiwanda
Upatikanaji wa soko	Uwezo wa kampuni au nchi kuuza bidhaa au huduma zake ndani na nje ya nchi
Ufikiwaji wa soko	Kipimo cha kiwango ambacho bidhaa au huduma inatumiwa na wateja ikilinganishwa na ukubwa wa soko linalokadiriwa kwa bidhaa au huduma hiyo.
Viwanda vya kimkakati	Viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika katika kutengeneza bidhaa nyingine, kuzalisha ajira za moja kwa moja kuanzia watu 2,000, kuongeza thamani ya madini adimu, na kuzalisha bidhaa ambazo zaidi ya asilimia 80 zitauzwa nje ya nchi
Uongezaji thamani	Hatua katika mchakato wa uzalishaji inayoboresha bidhaa au huduma ili kuongeza thamani yake
Mnyororo wa thamani	Muunganiko wa shughuli mbalimbali za uongezaji thamani katika bidhaa au huduma kuanzia uzalishaji hadi kumfikia mlaji
Wadau	Sekta binafsi, kampuni ya umma, wabia wa maendeleo, mashirika ya kimataifa, AZAKI na AZISE wenye nia ya kushiriki ama wanaoshiriki katika maendeleo ya viwanda

1. UTANGULIZI

1.1 Umuhimu wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera

Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda 2025 umeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Sera. Sera hiyo imetungwa kwa lengo la kuchochea maendeleo ya viwanda nchini Tanzania huku ikizingatia mabadiliko mapya ya kiuchumi duniani.

Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda 1996–2020 umewezesha kupatikana kwa mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na thamani ya bidhaa zilizotengenezwa viwandani kuongezeka kutoka shilingi milioni 254,326 mwaka 1996 hadi kufikia shilingi milioni 13,182,066 mwaka 2023; kiwango cha ukuaji wa shughuli za uzalishaji kwa mwaka kuongezeka kutoka asilimia 4.8 mwaka 1996 hadi asilimia 5.8 mwaka 2019; na mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa kuongezeka kutoka asilimia 1.1 mwaka 1996 hadi kufikia asilimia 7.0 mwaka 2023.

Licha ya mafanikio yaliyotajwa hapo juu, sekta ilikabiliwa na changamoto za kisera ambazo zilihitaji kushughulikiwa ili kuharakisha maendeleo ya viwanda. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kumalizika kwa kipindi cha utekelezaji wa Sera licha ya malengo yake kuendelea kutekelezwa, baadhi ya malengo kama ubinafsishaji yalipaswa kuondolewa katika sera kwa kuwa utekelezaji wake umekamilika; kuwapo kwa masuala kadhaa yanayoibuka kama maendeleo ya kiteknolojia; na usanifu wa sera kujumuisha masuala ya sekta nyingine kama vile sera ya fedha na kodi ambayo sekta haiwezi kuyashughulikia kikamilifu.

Kwa muktadha huo, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda 2025 imeandaliwa mkakati wa utekelezaji ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya Sera hiyo. Aidha, kupitia mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa mkakati, maendeleo ya utekelezaji wa Sera yatafuatiliwa, maeneo yanayohitaji maboresho yatabainishwa, na taarifa zitatolewa kwa wadau.

1.2 Masuala ya Utekelezaji

Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 2025 utaongoza utekelezaji wa afua mbalimbali katika maeneo matano ya Kisera. Maeneo hayo ni uongezaji thamani na mnyororo wa thamani; viwanda vya kimkakati; upatikanaji na ufikiaji wa soko; utafiti na ubunifu; na masuala mtambuka yanayojumuisha mazingira, jinsia, vijana, na watu wenye ulemavu, utawala bora, VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa.

1.3 Majukumu ya Taasisi na Wadau

Utekelezaji wa Sera hii ni jumuishi, ambapo wadau mbalimbali katika ngazi za kitaifa, kikanda, kimataifa pamoja na sekta binafsi watashiriki. Wizara yenye dhamana na maendeleo ya viwanda; wizara za kisekta; idara na wakala wa serikali; sekretarieti za mikoa; na mamlaka za serikali za mitaa zitasimamia utekelezaji wa sera kulingana na majukumu yalivyoanishwa. Wadau wengine muhimu ni sekta binafsi, washirika wa maendeleo, taasisi za elimu na utafiti, asasi zisizo za serikali, asasi za kiraia, vyombo vya habari, na jamii kwa ujumla. Wadau hawa wana jukumu na wajibu katika utekelezaji wa Sera kupitia utafiti, ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa viwanda, uhamasishaji, ufuatiliaji, utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya viwanda, na kujenga uwezo katika uendelezaji wa viwanda.

1.4 Matokeo Yanayotarajiwa

Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 2025 unatoa mwongozo wa namna ya kufikia lengo kuu la utekelezaji wa Sera, ambalo ni kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika maendeleo ya uchumi wa nchi. Hivyo, matokeo yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji madhubuti na wenye ufanisi wa mkakati huu ni pamoja na ongezeko la fursa za ajira, mapato ya serikali, mapato ya fedha za kigeni; kuchangia kukua kwa sekta nyingine; kuongeza thamani ya malighafi za asili; na kupungua kwa upotevu wa mazao baada ya mavuno, hususani mazao ya kilimo, mifugo, na uvuvi.

1.5 Hitimisho

Mkakati huu wa utekelezaji unatoa mwongozo wa namna Sera iliyorekebishwa itavyotekelezwa kwa ufanisi ili kukidhi mahitaji ya Sekta. Hivyo, kupitia utekelezaji wa afua mbalimbali zilizoainishwa katika Mkakati huu, nchi itashuhudia maendeleo ya uchumi yanayoongozwa na sekta ya viwanda, hususani kuongezeka kwa mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa na kuongezeka kwa tija katika sekta zinazohusiana na viwanda.

2. HALI ILIVYO

Wakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020, malengo mahususi yalikuwa ni kuboresha maendeleo ya watu kwa kuzalisha ajira, kuchochea mageuzi ya kiuchumi, kuboresha urari wa malipo, kuimarisha uhifadhi wa mazingira, kuwezesha maendeleo jumuishi, kukuza uwezo wa viwanda vipya, na kuimarisha viwanda mama. Hali ya utekelezaji wa Sera imefafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

2.1 Uongezaji wa Thamani na Mnyororo wa Thamani

Tanzania ina rasilimali za aina mbalimbali kama vile, mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini na misitu zinazopatikana nchini kote. Ili kutumia fursa zitokanazo na maliasili hizo, Serikali kwa kushirikiana na wadau, walianzisha na kutekeleza mikakati na mipango kadhaa ikiwamo Mkakati Unganishi wa Maendeleo ya Viwanda 2011–2025, Mkakati wa Maendeleo ya Alizeti 2016–2020, Mkakati wa Maendeleo ya Ngozi 2016–2020, Mkakati wa Maendeleo wa Nguo kutoka kwenye Pamba 2016–2020, Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Jamii ya Kunde 2016-2020, Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (Awamu I na II), na kutungwa kwa sheria mbalimbali.

Pamoja na mikakati na mipango hiyo, jitihada zingine zilizofanyika ni kuanzisha na kuboresha utendaji wa taasisi zinazosaidia uongezaji wa thamani wa rasilimali, kama vile Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania, Bodi ya Tumbaku Tanzania, Bodi ya Sukari Tanzania, Bodi ya Pamba Tanzania, Bodi ya Korosho Tanzania, Bodi ya Kahawa Tanzania, Bodi ya Nyama Tanzania, Bodi ya Maziwa Tanzania, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Tume ya Madini Tanzania, na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Taasisi hizi zilianzishwa ili kuwa na mchango katika kusimamia mnyororo wa thamani na ongezeko la thamani la mazao mbalimbali.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili la sera ni pamoja na kuanzishwa kwa viwanda nane (8) vya nguo na mavazi ambavyo kwa mwaka vinasokota tani 36,742; kusuka mita milioni 145; kufuma tani 7,920; na kutengeneza nguo na mavazi milioni 43. Aidha, viwanda vitatu (3) vya sukari vilianzishwa na vinne (4) viliboreshwa. Viwanda hivyo vinauwezo wa kuzalisha jumla ya tani 460,200 za sukari kwa mwaka. Vilevile, viwanda 11 vya saruji vilianzishwa na vitatu (3) viliboreshwa ambavyo kwa jumla vinaweza kuzalisha wastani wa tani 9,107,973 za saruji kwa mwaka. Pia, viwanda mbalimbali vilianzishwa, vikiwamo viwili (2) vya marumaru vinavyotengeneza mita za mraba milioni 18 kwa mwaka; viwanda 23 vya mbolea; viwanda tisa (9) vya usindikaji wa ngozi, vyenye uwezo wa kusindika vipande milioni 2.5 kwa mwaka; viwanda 16 vya usindikaji wa samaki; viwanda 17 vya kuzalisha mafuta ya kula; na viwanda vinne (4) vya vioo vinavyotengeneza tani 292,800 za vioo kwa mwaka.

Licha ya mafanikio hayo, Tanzania bado inauza kiasi kidogo cha bidhaa zilizoongezwa thamani. Aidha, kuna hasara zitokanazo na kukosekana kwa ufanisi katika uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini na misitu. Hali hii inasababishwa na upungufu wa wataalamu wenye ujuzi, miundombinu wezeshi kwa maendeleo ya viwanda vya uongezaji thamani na mnyororo wa thamani isiyotosheleza, na upungufu wa mitaji. Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hizo ipasavyo, msukumo mpya wa kisera unahitajika.

2.2 Viwanda vya Kimkakati

Viwanda vya kimkakati huzalisha bidhaa zinazotumika katika utengenezaji wa bidhaa nyingine. Pia, huchangia kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa ajira na bidhaa za kuuza nje na uongezaji thamani kwenye madini adimu. Viwanda vya kimkakati ni pamoja na viwanda vya uundaji na utengenezaji wa mashine na mitambo, uzalishaji wa kemikali, uzalishaji wa mikrochipu, uongezaji thamani kwenye madini adimu, utengenezaji wa nguo na mavazi, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya ulinzi, na uundaji na utengenezaji wa magari.

Ili kukuza uanzishwaji wa viwanda vya kimkakati, Serikali ilirekebisha na kuboresha ufanisi wa Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Mitambo cha Kilimanjaro (KMTC) kwa kuimarisha uwezo wake wa kutengeneza mashine za kuchakata mazao ya misitu, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo, na kutengeneza vipuri muhimu kwa ajili ya mashine za uchimbaji madini na ujenzi. Jitihada ziingine ni ukamilishaji wa utekelezaji wa mradi unganishi wa kuzalisha chuma wa Mchuchuma na Liganga na mradi wa kuzalisha magadisoda wa Engaruka.

Aidha, ukarabati wa vituo sita (6) vya kuendeleza teknolojia vya SIDO na karakana ya TEMDO ulifanyika. Ukarabati huo ulihusisha usimikaji wa mashine za kisasa kwa ajili ya utengenezaji wa mitambo inayotumika katika shughuli za kilimo, ujenzi na uchakataji wa madini. Vilevile, jumla ya viwanda 13 vya kuunganisha magari vilianzishwa, ambapo viwanda 11 ni vya kuunganisha matela ya kusafirishia mizigo na viwili (2) ni vya kuunganisha magari ya kubeba mizigo, ikiwa ni pamoja na malori na matipa. Kwa upande wa viwanda, vinavyohitaji nguvukazi nyingi viwanda nane (8) vya nguo na mavazi vilianzishwa, vikizalisha ajira za moja kwa moja 15,300 na zisizo za moja kwa moja 45,000.

Licha ya mafanikio yaliyobainishwa hapo juu, bado kuna fursa ambazo hazijatumika katika maeneo mbalimbali kama vile uchimbaji na uchakataji wa chuma ghafi na chuma cha pua, uundaji na utengenezaji wa mashine na mitambo, uundaji na uunganishaji wa magari, uzalishaji wa kemikali, utengenezaji wa dawa za binadamu na vifaa tiba, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya uzalishaji wa nishati, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya ulinzi na uzalishaji wa chipu. Maeneo mengine yenye fursa nyingi ni uzalishaji wa mitambo na vifaa vya elektroniki na mawasiliano; uzalishaji wa mitambo inayotumia akili unde; na uzalishaji wa zana za kilimo na mitambo ya uchakataji wa mazao ya kilimo, uvuvi, mifugo na na misitu; na uzalishaji wa nguo na mavazi pamoja na ngozi na bidhaa za ngozi.

Pia, viwanda vya kimkakati vilivyopo nchini vinatumia teknolojia za zamani, na hivyo kuzalisha bidhaa ambazo haziwezi kushindana na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa katika nchi zilizoendelea kiteknolojia. Hali hii inasababisha nchi kutegemea zaidi kuagiza vipuri, mashine, madawa ya binadamu na mifugo; na bidhaa za kati kutoka nje. Hivyo, marekebisho ya Sera yanahitajika ili kukabiliana na changamoto hizo.

2.3 Upatikanaji na Ufikiwaji wa Soko

Katika kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa za viwandani, Serikali imefanya jitihada mbalimbali zinazolenga masoko ya ndani na ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uuzaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani na kuboresha njia za usambazaji za ndani, kikanda na kimataifa. Kuhusu soko la ndani, jitihada muhimu zilizofanywa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya viwanda na masoko ya ndani, kuboresha miundombinu ya masoko, kuimarisha minyororo ya usambazaji kwa wazalishaji wa ndani, kuanzisha maeneo ya viwanda, na kuandaa maonesho ya biashara.

Katika soko la kimataifa, Serikali imefanya jitihada za kuimarisha ujumuishaji wa biashara kupitia makubaliano baina ya nchi, ya kikanda na ya kimataifa. Ili kutekeleza makubaliano hayo, Serikali imeridhia itifaki na kuingia mikataba mbalimbali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA), na Shirika la Biashara Duniani (WTO). Itifaki zilizoridhiwa ni pamoja na Itifaki ya Soko la Pamoja la EAC; Itifaki ya Umoja wa Forodha wa EAC; Itifaki ya EAC ya Afya na Usafi wa Chakula (SPS); na Itifaki ya Viwango, Uthibiti Ubora na Vipimo. Kupitia mtangamano wa kibiashara, katika mwaka 2023, mauzo ya nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 1,414.9 kwa soko la EAC, dola za Marekani milioni 1,727.5 kwa soko la SADC, dola za Marekani milioni 1,498.3 kwa soko la Umoja wa Ulaya (EU), dola za Marekani milioni 2,924.1 kwa soko la Asia, na dola za Marekani milioni 80.4 kwa soko la Marekani.

Licha ya mafanikio yaliyotajwa hapo juu, nchi inaagiza zaidi bidhaa zilizozalishwa viwandani kuliko inavyouza katika masoko ya nje. Hali hii inachangiwa na masuala kadhaa, ikiwa ni pamoja na uhaba wa ujuzi wa masoko, hususani kwenye eneo la majadiliano ya kibiashara, na miundombinu ya masoko isiyotosheleza. Changamoto zingine ni wazalishaji kutozingatia viwango vya soko; uwezo mdogo wa kutumia fursa za upendeleo zinazotokana na makubaliano ya mitangamano; na kushindwa kufikisha bidhaa kwa walaji kwa wakati. Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hizo ipasavyo, msukumo mpya wa kisera unahitajika.

2.4 Utafiti na Ubunifu

Utafiti na ubunifu katika maendeleo ya viwanda unahusisha ubunifu wa mawazo mapya yanayowezesha uundaji wa teknolojia mpya, mifumo ama uboreshaji wa teknolojia iliyopo na kwa matumizi ya viwandani na kuisambaza ili kuimarisha na kuboresha uzalishaji wa bidhaa za viwandani. Utafiti na ubunifu una mchango mkubwa katika uchumi wa kisasa kutokana na ongezeko la maarifa mapya na matumizi yake. Katika kufanikisha shughuli za utafiti na ubunifu, Serikali imeimarisha utendaji wa taasisi mbalimbali zikiwamo TEMDO; CAMARTEC; TIRDO; vyuo vikuu vya umma na binafsi; na taasisi za utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi. Kupitia jitihada hizo, mafaniko mbalimbali yamejitokeza, ambapo teknolojia 620 zilizobuniwa na taasisi hizo zimesambazwa na zinaendelea kutumika. Vilevile, programu 12 za viatamizi zilianzishwa ili kuwasaidia wabunifu kuendeleza teknolojia zao na kuzifanya zitumike kibiashara.

Licha ya jitihada zilizofanywa na Serikali, utafiti na ubunifu bado ni wa kiwango cha chini. Hali hii inasababishwa na upungufu wa miundombinu ya utafiti na ubunifu, uwekezaji mdogo katika utafiti na ubunifu, motisha kidogo kwa watafiti, uchache wa watafiti, kutokwenda na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, na kukosekana kwa muunganiko kati ya viwanda na taasisi za utafiti. Hivyo, marekebisho ya Sera yanahitajika.

2.5 Masuala Mtambuka

2.5.1 Wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu

Tanzania ina nguvukazi ya watu 25,861,023 ambapo asilimia nne (4) ndio wanaopata nafasi ya kuajiriwa viwandani. Ufinyu huo wa ajira unaleta changamoto zaidi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kuinua na kutumia vipaji vya ujasiriamali miongoni mwa makundi maalumu ili kuwajumuisha kwenye sekta ya viwanda ni muhimu katika kuendeleza makundi haya. Mahitaji ya msingi ya kujenga ushiriki wenye ufanisi wa makundi maalumu kwenye sekta ni kutambua mahitaji yao maalumu katika ngazi tofauti za viwanda, kuanzia uanzishwaji hadi ukuaji wake, na kuyajumuisha kwenye Sera. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa viwanda inaendeleza jitihada za kujumuisha masuala ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika maendeleo ya viwanda. Hivyo, marekebisho ya Sera yataongeza msukumo wa ushirikishwaji wa makundi hayo maalumu.

2.5.2 Uhifadhi wa mazingira

Maendeleo ya sekta ya viwanda nchini ni muhimu katika ukuaji wa uchumi, ingawa viwanda vinaweza kuchangia kufanya uchafuzi wa mazingira ambao una athari hasi kwa afya ya binadamu na mazingira. Mathalani, uchafuzi wa mazingira utokanao na gesi ya ukaa nchini Tanzania uliongezeka kutoka 435.30 Gg mwaka 1996 mpaka kufikia 696.58 Gg mwaka 2005 na kuchangia kuongeza madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi katika dunia. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kulinda na kuhifadhi mazingira katika sekta ya viwanda, zikiwamo kuanzishwa kwa mfumo wa kisheria na kitaasisi wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Licha ya jitihada hizo, sekta bado inakabiliwa na changamoto za uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda zisizozingatia utumiaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira. Hivyo, jamii inahitaji elimu zaidi kuhusu hatua za kuchukua ili kulinda mazingira kutokana shughuli za maendeleo ya viwanda, ambazo zinatakiwa kujumuishwa katika Sera kwa kuwajengea uwezo wenye viwanda.

2.5.3 VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa

Shughuli za viwanda hukutanisha makundi makubwa na tofauti ya watu zikihusisha wafanyakazi, watoa huduma, na wadau wengine ambao mwingiliano wao wa mara kwa mara unaweza kuongeza hatari ya kuenea kwa VVU/UKIMWI. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imefanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na VVU/UKIMWI katika shughuli za viwanda. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kujenga uelewa wa wadau kuhusu masuala ya VVU/UKIMWI.

Aidha, shughuli za viwanda husababisha watu kupata msongo wa mawazo, sonona na ulaji usiozingatia kanuni za afya, kutopumzika vya kutosha na hivyo kuwa katika hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukizwa kama vile shinikizo la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na figo. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imefanya jitihada za kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya viwanda. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kujenga uelewa wa wadau kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa.

3. DIRA, DHAMIRA, NA MALENGO

3.1 Dira

Kuwa na uchumi shindani, endelevu na jumuishi unaoongozwa na maendeleo ya viwanda.

3.2 Dhamira

Kuhamasisha maendeleo endelevu ya viwanda kwa kuongeza thamani ya malighafi na kuboresha minyororo ya thamani; kuwekeza kwenye utafiti na ubunifu; na kuendeleza viwanda vya kimkakati.

3.3 Malengo

Lengo Kuu

Kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

Malengo mahususi

Malengo mahususi ya Sera hii ni:

i. Kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine;
ii. Kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati;
iii. Kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa zilizozalishwa viwandani ndani na nje ya nchi;
iv. Kuwezesha utafiti na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda; na
v. Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za uendelezaji viwanda.

4. MALENGO YA SERA, MIKAKATI, NA SHABAHA

4.1 Uongezaji Wa Thamani na Mnyororo wa Thamani

Lengo

Kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine

Mikakati

i. Kujenga viwanda na kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu mipya ya viwanda na kuboresha miundombinu iliyopo;
ii. Kutoa mafunzo na kuanzisha programu za kuwajengea uwezo wafanyakazi;
iii. Kuanzisha na kuendeleza taasisi za kifedha kwa ajili ya uwekezaji katika viwanda;
iv. Kuhimiza matumizi ya rasilimali za ndani (rasilimali watu, huduma na malighafi) katika minyororo ya thamani na uongezaji thamani; na
v. Kuhamasisha uanzishwaji wa mifumo ya kulinda mitaji iliyowekezwa katika maendeleo ya viwanda wakati wa dharura.

Shabaha

i. Viwanda vipya 40 vyenye kutumia teknolojia ya kisasa kuanzishwa na kufanya kazi ifikapo Juni 2035;
ii. Maeneo mapya 15 ya viwanda yenye miundombinu ya kisasa kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
iii. Mfuko maalumu wa maendeleo ya viwanda kuanzishwa na kufanya kazi ifikapo Juni 2027;
iv. Wafanyakazi wa viwandani wapatao 1,000,000 kupatiwa ujuzi maalumu kuhusu uongezaji thamani ifikapo Juni 2035;
v. Moduli za mafunzo ya ujuzi maalumu katika uongezaji thamani kujumuishwa katika mitaala ya ufundi stadi ifikapo Juni 2027;
vi. Taasisi za kifedha zinazotoa huduma za kifedha kwa ajili ya maendeleo ya viwanda kuongezeka kwa asilimia 20 ifikapo Juni 2035;
vii. Miradi ya viwanda inayofadhiliwa kwa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi kuongezeka kwa asilimia 30 ifikapo Juni 2035;
viii. Ushiriki wa wawekezaji wazawa katika uongezaji thamani kuongezeka kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2035;
ix. Matumizi ya bidhaa zinazoongezewa thamani nchini katika miradi mikubwa ya kimkakati kuongezeka kwa asilimia 70 ifikapo Juni 2035; na
x. Mfumo wa kulinda mitaji iliyowekezwa katika maendeleo ya viwanda wakati wa dharura kuanzishwa ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

i. Mabadiliko ya kiwango cha upotevu wa mazao baada ya mavuno katika asilimia; na
ii. Mabadiliko katika ajira zilizozalishwa katika asilimia.

4.2 Viwanda vya Kimkakati

Lengo

Kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati.

Mikakati

i. Kuendeleza maeneo maalumu ya viwanda na vituo vya ubunifu ili kuwezesha kukua kwa viwanda vya Kimkakati;
ii. Kujenga na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vipya vya kimkakati na kuboresha viwanda vilivyopo; na
iii. Kuhamasisha upatikanaji wa ardhi iliyoendelezwa kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kimkakati.

Shabaha

i. Viwanda 35 vya kuunda na kuzalisha mashine/mitambo na vifaa kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
ii. Viwanda 12 vya kuzalisha kemikali na madawa kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
iii. Viwanda sita (6) vya kuunganisha magari vinafanya uzalishaji ifikapo Juni 2035;
iv. Viwanda 20 vya kuunda na kuzalisha vipuri vya mashine na magari kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
v. Viwanda vitatu (3) vya kuunda magari kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
vi. Viwanda 30 vya kimkakati vinavyoendana na miundombinu ya kimkakati kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
vii. Thamani ya mauzo ya nje ya viwanda vya kimkakati kuongezeka kwa asilimia 40 ifikapo Juni 2035;
viii. Viwanda 18 vya kuunda na kuzalisha samani na vyombo vya majumbani kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
ix. Viwanda 35 vya kuzalisha malighafi za ujenzi kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
x. Viwanda vitano (5) vya kuunda na kuzalisha roboti na mikrochipu kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
xi. Madini adimu mapya matano (5) yanayotumika kwa ajili ya viwanda vya kimkakati kuongezwa thamani ifikapo Juni 2035;
xii. Upatikanaji wa ardhi iliyotengwa na kuendelezwa kwa ajili ya viwanda vya kimkakati kwa kila Mkoa ifikapo Juni 2035;
xiii. Idadi ya viwanda vya kimkakati vilivyoanzishwa na sekta binafsi kuongezeka kwa asilimia 30 ifikapo Juni 2035; na
xiv. Miundombinu ya usafirishaji na kidijitali kwa ajili ya viwanda vya kimkakati kuongezeka kwa asilimia 30 ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

Mabadiliko ya gharama (shilingi trilioni) za bidhaa ghafi, kemikali, mitambo, vipuri, mafuta ya kula, dawa za binadamu na vifaa tiba, plastiki, na mashine zinazoagizwa.

4.3 Upatikanaji na Ufikiwaji wa Soko

Lengo

Kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa zilizozalishwa viwandani ndani na nje ya nchi.

Mikakati

i. Kujenga na kuendeleza miundombinu ya masoko;
ii. Kujenga uwezo wa rasilimali watu kuhusu utafutaji wa masoko mapya na ufikiaji wa masoko yaliyopo; na
iii. Kuimarisha intelijensia ya masoko na kuchochea ukuaji wa biashara.

Shabaha

i. Mauzo ya bidhaa yatokanayo na viwanda vya ndani kuongezeka kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2035;
ii. Uanuwai wa bidhaa zitokanazo na viwanda vya ndani zinazouzwa nje kuongezeka kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2035;
iii. Viwanda vilivyopata ithibati za kimataifa kuongezeka kwa asilimia 50 ifikapo Juni 2035;
iv. Wataalamu 10,000 kupatiwa mafunzo katika nyanja za masoko ya kimataifa na usimamizi wa mauzo ya nje ifikapo Juni 2035;
v. Mikataba mipya 50 ya kibiashara yenye masharti nafuu kuingiwa ifikapo Juni 2035; na
vi. Idadi ya viwanda vinavyofanya biashara-mtandao kuongezeka kwa asilimia 70 ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

Mabadiliko katika thamani ya mauzo ya nje katika dola za Marekani.

4.4 Utafiti na Ubunifu

Lengo

Kuwezesha utafiti na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda

Mikakati

i. Kuhamasisha na kuanzisha miundombinu mipya ya utafiti na ubunifu wa maendeleo ya viwanda pamoja na kuboresha iliyopo;
ii. Kujenga uwezo wa rasilimali watu kwa ajili ya utafiti na ubunifu wa maendeleo ya viwanda; na
iii. Kuimarisha muunganiko miongoni mwa wadau wa utafiti na ubunifu wa maendeleo ya viwanda.

Shabaha

i. Vituo vipya 10 vya ubunifu kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035;
ii. Kuongezeka kwa kiasi cha fedha zinazotengwa kwenye ufadhili wa serikali kwa ajili ya utafiti katika maendeleo ya viwanda ifikapo Juni 2035;
iii. Maeneo maalumu 10 ya viwanda na ubunifu kutengwa na kuendelezwa kwa ajili ya viwanda vya kimkakati ifikapo Juni 2031;
iv. Miradi 100 ya utafiti na ubunifu inayoendeshwa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo Juni 2035;
v. Taasisi 3 za utafiti na ubunifu katika maendeleo ya viwanda kuimarishwa ifikapo Juni 2035;
vi. Teknolojia 200 za kuongeza thamani kuhaulishwa na kutumika ifikapo Juni 2035;
vii. Nafasi 500 za kufanya tafiti zinazohusu maendeleo ya viwanda kufadhiliwa ifikapo Juni 2035;
viii. Fursa 1,000 za ufadhili wa masomo katika ujuzi maalumu viwandani kutolewa ifikapo Juni 2035;
ix. Mikataba 20 ya uhaulishaji teknolojia kati ya Tanzania na nchi nyingine kuingiwa ifikapo Juni 2035;
x. Hataza 300 za teknolojia za viwandani kutolewa ifikapo Juni 2035;
xi. Asilimia 30 ya viwanda vya kimkakati kutumia teknolojia za kisasa kama vile akili unde ifikapo Juni 2035; na
xii. Miradi 200 ya ushirikiano kati ya viwanda, taasisi za kitaaluma na serikali kutekelezwa ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

i. Mabadiliko katika uanuwai wa bidhaa za viwandani kwa asilimia
ii. Mabadiliko katika kiwango cha ubora wa bidhaa

4.5 Masuala Mtambuka

Lengo

Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za maendeleo ya viwanda

Mikakati

i. Kuhamasisha uzingatiaji wa utawala bora katika shughuli za maendeleo ya viwanda;
ii. Kujenga uwezo wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kuhusu uendeshaji wa shughuli za viwanda;
iii. Kujenga uelewa wa usimamizi wa mazingira katika shughuli za viwanda;
iv. Kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa katika shughuli za maendeleo ya viwanda; na
v. Kuhimiza matumizi ya mbinu za uzalishaji viwandani zenye kutunza mazingira.

Shabaha

i. Wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu 1,000,000 kupatiwa mafunzo kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa viwanda ifikapo Juni, 2035;
ii. Wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu 3,000,000 kuunganishwa na fursa za viwanda ifikapo Juni, 2035;
iii. Viwanda 200 kupatiwa mafunzo kuhusu mbinu za kutumia teknolojia endelevu na rafiki kwa mazingira ifikapo Juni 2035;
iv. Asilimia 60 ya wafanyakazi wa viwandani kuhamasishwa kufanya uchunguzi wa afya ifikapo Juni 2035;
v. Wafanyakazi 1,500,000 wa viwandani kupatiwa elimu ya afya kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa na VVU/UKIMWI na tiba ifikapo Juni 2035; na
vi. Wafanyakazi 1,000,000 kupatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya rasilimali rafiki kwa mazingira ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

i. Mabadiliko katika kiwango cha ushiriki wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika maendeleo ya viwanda kwa asilimia;
ii. Mabadiliko ya viwanda vinavyozingatia vigezo vya utunzaji wa mazingira kwa asilimia; na
iii. Mabadiliko katika viwango vya maambukizi ya VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa.

5. MFUMO WA KITAASISI

Wadau wakuu katika utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025 ni: Wizara yenye dhamana ya Viwanda; Wizara za kisekta, Taasisi za Serikali zilizo chini ya Wizara za kisekta; Sekretarieti za Miko; na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wadau wengine ni Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Elimu na Utafiti, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Asasi Zisizo za Serikali.

Majukumu na wajibu wa wadau wa utekelezaji wa Sera yameainishwa katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Wajibu na Majukumu ya Wadau

Na	Jina la Mdau	Wajibu na Majukumu
1.	Wizara yenye dhamana ya Viwanda	Kutekeleza na kuratibu utekelezaji wa Sera na mkakati ili kuendeleza sekta ya viwanda
2.	Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Kutoa mwongozo kuhusu miundo ya taasisi na masuala yanayohusiana na rasilimali watu
3.	Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji	Kutoa mwongozo kuhusu mipango ya maendeleo ya Taifa
4.	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)	Kuratibu shughuli za maendeleo ya viwanda katika ngazi za mikoa na Serikali za mitaa
5.	Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira	Kuhifadhi na kusimamia mazingira kwa ajili ya maendeleo ya viwanda
6.	Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu	Kuratibu utekelezaji na ufuatiliaji wa Sera
7.	Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu	Kutoa mwongozo jumuishi wa masuala ya stahiki za rasilimali watu, usalama na afya mahali pa kazi na makundi maalumu
8.	Wizara yenye dhamana ya Fedha	Kutoa na kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha na vivutio kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
9.	Wizara yenye dhamana ya Ardhi	Kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
10.	Wizara yenye dhamana ya Kilimo	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za mazao ya kilimo zenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
11.	Wizara yenye dhamana ya Mifugo	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za mazao ya mifugo zenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
12.	Wizara yenye dhamana ya Uvuvi	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za mazao ya uvuvi yenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
13.	Wizara yenye dhamana ya Nishati	Kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya kutosha na yenye uhakika kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
14.	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje	Kuratibu diplomasia ya uendelezaji wa viwanda
15.	Wizara yenye dhamana ya Madini	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za madini zenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
.16.	Wizara yenye dhamana ya Uchukuzi	Kujenga na kuendeleza miundombinu (bandari, anga na reli) ili kukidhi mahitaji ya uendelezaji wa viwanda
17.	Wizara yenye dhamana ya Ujenzi	Kujenga na kuendeleza miundombinu ya barabara ili kukidhi mahitaji ya uendelezaji wa viwanda.
18.	Wizara yenye dhamana ya Maji	Kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
.19.	Wizara yenye dhamana ya Mawasiliano	Kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu ya mawasiliano kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
20.	Wizara yenye dhamana ya Katiba na Sheria	Kutoa mwongozo wa kisheria kwa ajili ya maendeleo ya viwanda
21.	Wizara yenye dhamana ya Elimu	Kuandaa wahitimu wenye ujuzi kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
22	Wizara yenye dhamana ya Sayansi na Teknolojia	Kuratibu masuala ya tafiti za kisayansi ili kuibua teknolojia kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
23	Wizara yenye dhamana ya Afya	Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
24	Wizara ya Maliasili na Utalii	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi zitokanazo na maliasili kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
25	Wizara yenye dhamana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	Kuhakikisha mazingira salama, kuunda teknolojia na kushiriki katika uendelezaji wa viwanda
26	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi	Kuhakikisha usalama wa nchi na kushiriki katika uendelezaji wa viwanda
27	Wizara yenye dhamana ya Habari, Utamaduni na Michezo	Kuhabarisha jamii kuhusu maendeleo ya viwanda nchini
28	Wizara yenye dhamana ya Jinsia na makundi maalumu	Kutoa mwongozo na kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya jinsia na makundi maalumu katika shughuli za uendelezaji wa viwanda
29	Sekretarieti za Mikoa	Kuratibu shughuli za uendelezaji wa viwanda katika ngazi za mikoa
30	Mamlaka za Serikali za Mitaa	Kutekeleza Sera katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa
31	Idara na Wakala za Serikali	Kutekeleza Sera katika maeneo yao ya mamlaka kwa kujumuisha shughuli za uendelezaji wa viwanda katika mipango, mikakati, na programu zao za maendeleo
32	Taasisi zilizo chini ya Wizara yenye dhamana ya viwanda	Kutekeleza Sera kulingana na majukumu yao ya kisheria
33	Washirika wa Maendeleo	Kushiriki katika kutekeleza Sera kwa kujenga uwezo wa kiufundi, kuchangia rasilimali fedha na teknolojia kwa uendelezaji wa viwanda

Na	Jina la Mdau	Wajibu na Majukumu
34	Taasisi za elimu ya juu na utafiti	Kufanikisha utekelezaji wa Sera kwa kutoa: mafunzo; ubunifu; na utafiti kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
35	Sekta Binafsi	Utekelezaji wa Sera kwa kuwekeza katika uendelezaji wa viwanda
36	Asasi Zisizo za Serikali na Asasi za Kiraia	Kushiriki katika uendelezaji wa viwanda kuhamasisha ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya viwanda.
37	Mashirika ya Kikanda na Kimataifa	Kushiriki katika kutekeleza Sera kwa kujenga uwezo wa kiufundi na kuchangia rasilimali.
38	Vyombo vya habari	Kuanda na kusambaza taarifa juu ya fursa za maendeleo ya viwanda zilizobainishwa katika Sera na utekelezaji wake.

6. UTEKELEZAJI WA SERA

Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 2025 unajumuisha rasilimali fedha zinazohitajika, muda wa utekelezaji, na wadau wakuu kama walioainishwa ili kufanikisha malengo kama inavyoelezwa katika Jedwali Na. 2.

6.1 Rasilimali Fedha Zinazohitajika

Jumla ya shilingi trilioni 76.96 zitahitajika ili kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 2025. Fedha hizo zitawezeshwa kupitia bajeti ya Serikali, sekta binafsi, na washirika wa maendeleo.

6.2 Muda wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Mkakati huu utakuwa wa kipindi cha miaka kumi (2025/2026–2034/2035), kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali Na. 2.

Jedwali 2: Mpango wa Utekelezaji (2025/26 - 2035/36)

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
1	Kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine	Kujenga viwanda na kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu mipya ya viwanda na kuboresha miundombinu iliyopo	Viwanda vipya 40 vyenye kutumia teknolojia ya kisasa kuanzishwa na kufanya kazi ifikapo Juni 2035	**4,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kutoa mafunzo na kuanzisha programu za kuwajengea uwezo wafanyakazi	Maeneo mapya 15 ya viwanda yenye miundombinu ya kisasa kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**60,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Wafanyakazi wa viwandani wapatao 1,000,000 kupatiwa ujuzi maalumu kuhusu uongezaji thamani ifikapo Juni 2035	**20,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kuanzisha na kuendeleza taasisi za kifedha kwa ajili uwekezaji katika viwanda	Moduli za mafunzo ya ujuzi maalumu katika uongezaji thamani kujumuishwa katika mitaala ya ufundi stadi ifikapo Juni 2027	**950**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Taasisi za kifedha zinazotoa huduma za kifedha kwa ajili ya maendeleo ya viwanda kuongezeka kwa asilimia 20 ifikapo Juni 2035	**2,450**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
			Mfuko maalumu wa maendeleo ya viwanda kuanzishwa na kufanya kazi ifikapo Juni 2027	**13,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Miradi ya viwanda inayofadhiliwa kwa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi kuongezeka kwa asilimia 30 ifikapo Juni 2035	**9,300**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kuhimiza matumizi ya rasilimali za ndani (rasilimali watu, huduma na malighafi) katika minyororo ya thamani na uongezaji thamani	Ushiriki wa wawekezaji wazawa katika uongezaji thamani kuongezeka kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2035	**3,450**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Matumizi ya bidhaa zinazoongezewa thamani nchini katika miradi mikubwa ya kimkakati kuongezeka kwa asilimia 70 ifikapo Juni 2035	**2,150**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
		Kuhamasisha uanzishwaji wa mifumo ya kulinda mitaji iliyowekezwa katika maendeleo ya viwanda wakati wa dharura	Mfumo wa kulinda mitaji iliyowekezwa katika maendeleo ya viwanda wakati wa dharura kuanzishwa ifikapo Juni 2035	**1,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
2	Kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati	Kuendeleza maeneo maalumu ya viwanda na vituo vya ubunifu ili kuwezesha kukua kwa viwanda vya Kimkakati	Idadi ya viwanda vya kimkakati vilivyoanzishwa na sekta binafsi kuongezeka kwa asilimia 30 ifikapo Juni 2035	**4,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Miundombinu ya usafirishaji na kidijitali kwa ajili ya viwanda vya kimkakati kuongezeka kwa asilimia 30 ifikapo Juni 2035	**10,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Thamani ya mauzo ya nje ya viwanda vya kimkakati kuongezeka kwa asilimia 40 ifikapo Juni 2035	**800**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kujenga na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vipya vya kimkakati na kuboresha viwanda vilivyopo	Viwanda 30 vya kimkakati vinavyoendana na miundombinu ya kimkakati kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**15,500,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
			Viwanda 18 vya kuunda na kuzalisha samani na vyombo vya majumbani kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**5,120,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Viwanda vitano (5) vinavyounda na kuzalisha roboti na mikrochipu kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**4,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Viwanda thelathini na tano (35) vya kuzalisha malighafi za ujenzi kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**400,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Viwanda sita (6) vya kuunganisha magari kuwa vinafanya uzalishaji ifikapo Juni 2035	**1,500**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
			Viwanda 20 vya kuunda na kuzalisha vipuri vya mashine na magari kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**7,608,660**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Viwanda vitatu (3) vya kuunda magari kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**7,500**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Viwanda 35 vya kuunda na kuzalisha mashine/mitambo na vifaa kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**6,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Viwanda 12 vya kuzalisha kemikali na madawa kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**4,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Madini adimu mapya matano (5) yanayotumika kwa ajili ya viwanda vya kimkakati kuongezwa thamani ifikapo Juni 2035	**5,000,000**	2025–2035	MIT PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MoF, ME, MM, MoA, MLHHS, MoLF, MNRT, MFA, MT, MW, MC, MEST MoHA, MCDGEC, MDA, LGAs, DPs, RGs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
		Kuhamasisha upatikanaji wa ardhi iliyoendelezwa kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kimkakati	Upatikanaji wa ardhi iliyotengwa na kuendelezwa kwa ajili ya viwanda vya kimkakati kwa kila Mkoa ifikapo Juni 2035	**100,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
3	Kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa zilizozalishwa viwandani ndani na nje ya nchi	Kujenga na kuendeleza miundombinu ya masoko	Mauzo ya bidhaa yatokanayo na viwanda vya ndani kuongezeka kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2035	**700**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Uanuwai wa bidhaa zitokanazo na viwanda vya ndani zinazouzwa nje kuongezeka kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2035	**1,000,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Viwanda viliivyopata ithibati za kimataifa kuongezeka kwa asilimia 50 ifikapo Juni 2035	**70,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kujenga uwezo wa rasilimali watu kuhusu utafutaji wa masoko mapya na ufikiaji wa masoko yaliyopo	Wataalamu 10,000 kupatiwa mafunzo katika nyanja za masoko ya kimataifa na usimamizi wa mauzo ya nje ifikapo Juni 2035	**600**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
			Idadi ya viwanda vinavyofanya biashara-mtandao kuongezeka kwa asilimia 70 ifikapo Juni 2035	**150**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kuimarisha intelijensia ya masoko na kuchochea ukuaji wa biashara	Mikataba mipya 50 ya kibiashara yenye masharti nafuu kuingiwa ifikapo Juni 2035	**450**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
4	Kuwezesha utafiti na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda	Kuhamasisha na kuanzisha miundombinu mipya ya utafiti na ubunifu wa maendeleo ya viwanda pamoja na kuboresha iliyopo	Vituo vipya 10 vya ubunifu kuanzishwa na kuendelezwa ifikapo Juni 2035	**5,129,050**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Kuongezeka kwa kiasi cha fedha zinazotengwa kwenye ufadhili wa serikali kwa ajili ya utafiti katika maendeleo ya viwanda ifikapo Juni 2035	**5,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Maeneo maalumu 10 ya viwanda na ubunifu kutengwa na kuendelezwa kwa ajili ya viwanda vya kimkakati ifikapo Juni 2031	**9,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
			Miradi 100 ya utafiti na ubunifu inayoendeshwa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo Juni 2035	**550**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Taasisi 3 za utafiti na ubunifu katika maendeleo ya viwanda kuimarishwa ifikapo Juni 2035	**2,900**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Teknolojia 200 za kuongeza thamani kuhaulishwa na kutumika ifikapo Juni 2035	**4,700**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kujenga uwezo wa rasilimali watu kwa ajili ya utafiti na ubunifu wa maendeleo ya viwanda	Nafasi 500 za kufanya tafiti zinazohusu maendeleo ya viwanda kufadhiliwa ifikapo Juni 2035	**280**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Fursa 1,000 za ufadhili wa masomo katika ujuzi maalumu viwandani kutolewa ifikapo Juni 2035	**280**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
			Mikataba 20 ya uhaulishaji teknolojia kati ya Tanzania na nchi nyingine kuingiwa ifikapo Juni 2035	**1,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kuimarisha muundaniko miongoni mwa wadau wa utafiti na ubunifu wa maendeleo ya viwanda	Hataza 300 za teknolojia za viwandani kutolewa ifikapo Juni 2035	**730**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Asilimia 30 ya viwanda vya kimkakati kutumia teknolojia za kisasa kama vile akili unde ifikapo Juni 2035	**7,600**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Miradi 200 ya ushirikiano kati ya viwanda, taasisi za kitaaluma na serikali kutekelezwa ifikapo Juni 2035	**450**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
5	Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za	Kuhamasisha uzingatiaji wa utawala bora katika shughuli za maendeleo ya viwanda	Wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu 1,000,000 kupatiwa mafunzo kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa viwanda ifikapo Juni, 2035	**1,200**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE

Na	Lengo	Mikakati	Shabaha	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Muda	Wahusika
	maendeleo ya viwanda	Kujenga uwezo wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kuhusu uendeshaji wa shughuli za viwanda	Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu milioni tatu (3,000,000) kuunganishwa na fursa za maendeleo ya viwanda ifikapo Juni 2035	**1,700**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kujenga uelewa wa usimamizi wa mazingira katika shughuli za viwanda	Viwanda 200 kupatiwa mafunzo kuhusu mbinu za kutumia teknolojia endelevu na rafiki kwa mazingira ifikapo Juni 2035	**600**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa katika shughuli za maendeleo ya viwanda	Asilimia 60 ya wafanyakazi wa viwandani kuhamasishwa kufanya uchunguzi wa afya ifikapo Juni 2035	**500**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
			Wafanyakazi 1,500,000 wa viwandani kupatiwa elimu ya afya kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa na VVU/UKIMWI na tiba ifikapo Juni 2035	**1,000**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		Kuhimiza matumizi ya mbinu za uzalishaji viwandani zenye kutunza mazingira	Wafanyakazi 1,000,000 kupatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya rasilimali rafiki kwa mazingira ifikapo Juni 2035	**500**	2025–2035	MIT, PO-RALG, PO-PI, VPO, PMO, MF, ME, MM, MA, MLHHS, MLF, MNRT, MFA, MT, MH, MoW, MW, MEST, MHA, MCDGWSG, RSs, MDA, LGAs, DPs, Sekta Binafsi, AZAKI, AZISE
		JUMLA		**76,960,000**		

7. UFUATILIAJI NA TATHMINI

7.1 Utangulizi

Sehemu hii inafafanua umuhimu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Sera na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu inayosaidia kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera. Nyenzo hii huwezesha Wizara yenye dhamana kupima ufanisi wa utekelezaji wa malengo yaliyobainishwa kwenye Sera. Aidha, mfumo huu husaidia Wizara yenye dhamana na viwanda kuratibu utekelezaji wa mikakati kwa kubuni programu mbalimbali. Sura hii inaelezea namna dira ya Sera itakavyofikiwa kupitia utekelezaji wa mkakati na namna wadau watakavyonufaika na utekelezaji huo. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini unaonyesha lengo kuu la mkakati, walengwa wa afua mbalimbali zitazotekelezwa, mpango wa ufuatiliaji, mapitio yaliyokusudiwa, mpango wa tathmini, na mpango wa utoaji taarifa.

Lengo kuu la Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ni kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mkakati ili kuongeza ufanisi na tija katika afua zinazotekelezwa. Malengo mahususi ya mfumo huu ni kama ifuatavyo:

(i) Kuweka viashiria vya kuwezesha tathmini ya utekelezaji;
(ii) Kuweka mwongozo wa ushiriki wa wadau katika shughuli za utekelezaji na ufuatiliaji; na
(iii) Kudhibiti matumizi ya rasilimali wakati wa utekelezaji.

7.2 Walengwa

Walengwa wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni wizara za kisekta, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, sekta binafsi, asasi za kiraia, taasisi za elimu na utafiti, na jamii kwa ujumla.

7.3 Mipango ya Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini

Sehemu hii inafafanua mipango ya ufuatiliaji, mapitio na tathmini kwa kipindi cha miaka 10 cha utekelezaji wa mkakati. Vilevile, sehemu hii inaeleza kuhusu mapitio ya Sera yatakayofanyika mara kwa mara; upimaji na tathmini ya ufanisi, tija, na manufaa; na uendelevu wa matokeo ya mpango.

7.3.1 Mpango wa ufuatiliaji

Ufuatiliaji utahusisha ukusanyaji endelevu wa data, uchambuzi, viashiria vya upimaji na muda wa uwasilishaji taarifa. Mpango huu utaiwezesha Wizara yenye dhamana na Viwanda pamoja na wadau kupata taarifa ya mwenendo wa utekelezaji kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji na kiwango cha matumizi ya fedha zilizotengwa katika kipindi maalumu.

7.3.2 Mpango wa mapitio

Mpango wa mapitio utatekelezwa na Wizara yenye dhamana na viwanda kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mpango huo utajumuisha mikutano, mapitio ya utekelezaji wa viashiria vya muda mfupi, na tathmini za haraka (papo kwa papo). Mpango utasaidia mamlaka husika kufanya uamuzi sahihi na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa wadau.

7.3.3 Mpango wa mapitio ya viashiria vya muda mfupi

Mpango huu unatumia vigezo vinavyotumika kubaini matukio muhimu katika ratiba, kama vile kukamilika kwa matukio makuu au hatua zilizoainishwa wakati wa upangaji. Hivyo, mapitio ya viashiria vya muda mfupi yanalenga kutathmini kiwango cha utekelezaji wa malengo kwa mwaka unaohusika na kubaini ikiwa utekelezaji huo uko katika mwelekeo sahihi au la. Taarifa ya mapitio haya itawezesha kufanya maboresho ya malengo na mikakati ya kuyafikia.

7.3.4 Mpango wa tathmini

Tathmini ya utekelezaji itafanyika kwa vipindi maalumu ili kubaini ufanisi na tija ya utekelezaji wa malengo. Mchakato wa tathmini utajikita katika kupima matokeo yaliyopatikana na manufaa yake kwa walengwa. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera, tathmini itafanyika kwa vipindi viwili, ambapo tathmini ya kwanza itafanyika baada ya miaka mitano na tathmini ya pili itafanyika baada ya miaka kumi. Tathmini zitapima kufikiwa kwa malengo na shabaha zilizoainishwa katika Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025. Vilevile, tathmini hizo zitabainisha changamoto za utekelezaji na kuzifanyia kazi. Viashiria vya ufuatiliaji na tathmini vimebainishwa katika Jedwali Na. 3.

Jedwali 3: Viashiria vya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi

Viashiria vya Matokeo ya Muda Mfupi	Viashiria vya Matokeo	Takwimu Msingi		Malengo		Chanzo
		Mwaka	Kiasi	Mwaka	Kiasi	
Lengo la kimkakati 1: Kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine						
Idadi ya viwanda vyenye kutumia teknolojia ya kisasa	Mabadiliko ya kiwango cha upotevu wa mazao	2024	49	2035	20	i. Ripoti ya Wizara ya Kilimo ii. Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania
Idadi ya maeneo mapya yenye miundombinu ya kisasa	baada ya mavuno katika asilimia					
Kiwango cha asilimia za taasisi za fedha zinazotoa huduma za kifedha katika viwanda						
Kuwapo kwa mfuko wa maendeleo	Mabadiliko katika ajira zilizozalishwa katika asilimia	2024	5.2	2035	9	i. Ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ii. Ripoti ya Utafiti wa Kitaifa wa Uchumi iii. Ripoti ya Ofisi ya Takwimu ya Taifa
Idadi ya wafanyakazi waliopatiwa ujuzi maalumu						
Kiwango cha asilimia za ushiriki wa wawekezaji wazawa katika uongezaji thamani						
Moduli za ujuzi maalumu zilizojumuishwa katika mitaala ya ufundi stadi						
Lengo la kimkakati 2: Kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati						
Idadi za viwanda vya kuunda magari	Mabadiliko ya ghafa-ma (shilingi trilioni) za bidhaa ghafi, kemikali, mitambo vipuri	2024	24	2035	12	i. Ripoti ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania ii. Ripoti ya Benki kuu ya Tanzania
Idadi za viwanda vya kuunganisha magari						
Kiwango cha asilimia ya viwanda vya kimkakati vilivyoanzishwa na Sekta binafsi						

Viashiria vya Matokeo ya Muda Mfupi	Viashiria vya Matokeo	Takwimu Msingi		Malengo		Chanzo
		Mwaka	Kiasi	Mwaka	Kiasi	
Lengo la kimkakati 3: Kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa ndani na nje ya nchi						
Idadi ya viwanda vya kimkakati vinavyounda na kutengeneza roboti na mikrochipu	Mabadiliko ya ghafa-ma (shilingi trilioni) za bidhaa ghafi, kemikali, mitambo, vipuri, mafuta ya kula, dawa za binadamu na vifaa tiba, plastiki, na mashine zinazoagizwa					
Kemikali za viwandani 5 kuendelezwa ifikapo Juni 2035.						
Idadi ya madini adimu yaliyongezewa thamani na kutumika kwa ajili ya viwanda vya kimkakati						
Kiwango cha asilimia ya thamani ya mauzo ya viwanda vya kimkakati nje ya nchi						
Idadi ya viwanda vya kimkakati vya kuongeza thamani ya madini						
Lengo la kimkakati 3: Kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa ndani na nje ya nchi						
Kiwango cha asilimia ya mauzo ya nje kinachochangiwa na bidhaa zitokanazo na viwanda vya ndani	Mabadiliko katika thamani ya mauzo ya nje katika dola za Marekani milioni	2024	1,363.3	2035	8,322	ii. Wizara ya Fedha ii. Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania iii. Ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara
Idadi ya wataalamu waliopatiwa mafunzo katika nyanja za masoko ya kimataifa na usimamizi wa mauzo ya nje						
Idadi ya mikataba mipya ya kibiashara yenye masharti nafuu iliyoingiwa						
Kiwango cha asilimia ya viwanda vilivyopata ithibati za kimataifa						
Kiwango cha asilimia ya mauzo ya bidhaa yatokanayo na viwanda vya ndani						

Viashiria vya Matokeo ya Muda Mfupi	Viashiria vya Matokeo	Takwimu Msingi		Malengo		Chanzo
		Mwaka	Kiasi	Mwaka	Kiasi	
Kiwango cha asilimia ya ongezeko la viwanda vinavyofanya biashara mtandao						
Lengo la kimkakati 4: Kuwezesha utafiti na ubunifu wa teknolojia za viwanda						
Idadi ya vituo vipya vya ubunifu vilivyoanzishwa	Mabadiliko katika uanuwai wa bidhaa za viwandani katika asilimia	2024	Zitapatikana baada ya utafiti msingi	2035	300	ii. Ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara
Idadi ya mikataba ya uhawilishaji teknolojia kati ya nchi na nchi iliyoingiwa.						
Idadi ya tafiti zilizofadhiliwa zinazohusu maendeleo ya viwanda	Mabadiliko katika kiwango cha ubora wa bidhaa	2024	N/A	2035	Itapimwa kwa sifa	i. Ripoti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia ii. Ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara
Idadi ya fursa za ufadhili wa masomo katika ujuzi maalum viwandani zilizotolewa						
Kiwango cha asilimia ya fedha zilizotengwa kwenye ufadhili wa serikali kwa ajili ya utafiti						
Kiwango cha asilimia za viwanda vya kimkakati vinavyotumia teknolojia za kisasa						
Idadi ya miradi ya utafiti iliyoanzishwa na kuendelezwa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi						
Idadi ya hataza za teknolojia za viwandani zilizotolewa						
Idadi ya taasisi za utafiti na ubunifu zilizoimarishwa						

Viashiria vya Matokeo ya Muda Mfupi	Viashiria vya Matokeo	Takwimu Msingi		Malengo		Chanzo
		Mwaka	Kiasi	Mwaka	Kiasi	
Lengo la kimkakati 5: Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za maendeleo ya viwanda						
Idadi ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu waliopatiwa mafunzo	Mabadiliko katika kiwango cha ushiriki wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika maendeleo ya viwanda kwa asilimia	2024	Zitapatikana baada ya utafiti msingi	2035	20	i. Ripoti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ii. Ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara
Idadi ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu waliounganishwa na fursa za viwanda						
Idadi ya wafanyakazi wa viwandani waliopatiwa mafunzo kuhusu mbinu na teknolojia endelevu	Mabadiliko ya viwanda vinavyozingatia vigezo vya utunzaji wa mazingira kwa asilimia	2024	Zitapatikana baada ya utafiti msingi	2035	100	i. Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ii. Ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara
Idadi ya wafanyakazi wa viwandani waliopatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya rasilimali rafiki kwa mazingira						
Kiwango cha asilimia za wafanyakazi waliohamasishwa kufanya uchunguzi wa afya	Mabadiliko katika viwango vya maambukizi ya VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa	2024	Zitapatikana baada ya utafiti msingi	2035	Kitapatikana baada ya utafiti msingi	i. Ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ii. Ripoti ya Wizara ya Afya iii. Ripoti ya Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI iv. Ripoti ya Mamlaka ya Afya na Usalama Kazini Tanzania
Idadi ya wafanyakazi wa viwandani waliopatiwa elimu ya afya kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa na VVU/UKIMWI						

7.3.5 Mpango wa utoaji taarifa

Mpango huu utahusisha utoaji taarifa kuhusu mwenendo wa ufikiwaji wa malengo yaliyobainishwa katika Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025 ukilinganisha matumizi ya rasilimali na manufaa yaliyopatikana kwa walengwa. Aidha, mpango huu utahusisha utoaji wa taarifa ndani na nje ya Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya viwanda.

7.3.5.1 Mpango wa utoaji taarifa ndani ya Wizara

Mpango wa utoaji taarifa ndani ya Wizara unakusudia kutoa muhtasari wa maendeleo ya utekelezaji wa Sera. Kipekee, mpango huu utahusisha maandalizi ya aina nne za taarifa, yaani taarifa za maendeleo ya idara, taarifa za maendeleo ya miradi, taarifa za kila robo mwaka, na taarifa za kila mwaka. Taarifa hizi zitaandaliwa kila robo mwaka, kila mwaka, au kwa kadri itakavyohitajika.

7.3.5.2 Mpango wa utoaji taarifa nje ya Wizara

Mpango wa utoaji wa taarifa nje ya Wizara utahusisha maandalizi ya taarifa za fedha, taarifa za kila mwaka, taarifa za vipindi vya kati, na taarifa za matokeo ya utekelezaji. Utoaji wa taarifa hizi utabainisha aina ya taarifa, wapokeaji, muda wa utoaji taarifa na taasisi husika. Taarifa hizi zitawasilishwa kwa wadau kama vile Wizara, Bunge na umma kwa ujumla.

7.4 Ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu

Takwimu za ufuatiliaji na tathmini zitakusanywa mara kwa mara kwa kutumia zana za ufuatiliaji zilizokubaliwa na Wizara yenye dhamana na viwanda. Takwimu zitakusanywa kupitia tafiti, taarifa za utendaji, taarifa za shughuli mahususi, ziara za ufuatiliaji, na vyanzo vingine vinavyoaminika. Takwimu zitachambuliwa na kuingizwa kwenye kanzidata ya Taifa ya Viwanda.

7.5 Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

7.5.1 Aina za taarifa za ufuatiliaji na tathmini

Katika ngazi ya Wizara, taarifa mbalimbali zitatumika kufanya ufuatiliaji na tathmini kama ifuatavyo:

(i) Taarifa za Wizara yenye dhamana za kila robo mwaka, nusu mwaka na kila mwaka;
(ii) Taarifa za tathmini za wizara, idara na wakala za serikali, mashirika, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;
(iii) Taarifa za kila mwaka za washirika wa maendeleo; na
(iv) Taarifa za mapitio na tafiti mbalimbali.

7.5.2 Ratiba ya utoaji taarifa

Ratiba ya utoaji taarifa imebainishwa katika Jedwali Na.4.

Jedwali Na. 4: Ratiba ya Utoaji Taarifa

Aina ya Taarifa	Maudhui	Muda
Taarifa ya Kina ya Utekelezaji	Taarifa za kina zinazojumuisha shughuli zote zilizotekelezwa katika ngazi ya Wizara	Nusu mwaka na mwaka
Taarifa ya Tathmini	Taarifa za tathmini ya utekelezaji za ndani na nje ya Wizara	Miaka miwili na nusu, mitano, na miaka kumi
Mapitio ya Utekelezaji wa Sera	Mapitio ya utekelezaji wa Sera	Baada ya miaka mitano

7.5.3 Mfumo wa utoaji taarifa

Taarifa za utekelezaji zitaandaliwa na taasisi husika na kuwasilishwa kwa Wizara yenye dhamana na viwanda kwa ajili ya kuziunganisha. Aidha, Wizara itaandaa taarifa za utendaji na kuziwasilisha kwa wadau kila robo mwaka, nusu mwaka, na kila mwaka kwa hatua muhimu za utekelezaji.

7.5.4 Mfumo wa kutoa mrejesho

Mfumo wa utoaji mrejesho unahusisha utaratibu wa kutoa taarifa baina ya watekelezaji na watumiaji wa taarifa. Aidha, mrejesho utaimarisha ushirikiano baina ya wadau ili kuboresha taarifa na mifumo ya utoaji taarifa.

7.6 Matumizi ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitatumiwa na wadau ili:

(i) Kuwezesha utoaji bora wa huduma;
(ii) Kuboresha uwajibikaji kupitia matokeo yatakayopatikana;
(iii) Kufanya uamuzi sahihi;
(iv)Kuandaa mipango; na
(v) Kuwa na matumizi sahihi ya rasilimali.

7.7 Mpango wa Utekelezaji

Mpango wa kina wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda 2025 unaojumuisha maeneo matano ya kipaumbele yaliyobainishwa katika Sera na mkakati wake wa utekelezaji utaandaliwa mwanzoni mwa kipindi cha utekelezaji wa sera. Mikakati mbalimbali iliyobainishwa itaandaliwa ili kuainisha shughuli na gharama za utekelezaji.

Aidha, watekelezaji wa mpango watatumia njia shirikishi na jumuishi ili kufikia lengo kuu la Sera ambalo ni kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika maendeleo ya uchumi.

7.8 Hitimisho

Ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ni nyenzo muhimu zitakazotumiwa na Wizara yenye dhamana na viwanda na wadau wengine kufanya uamuzi na kuimarisha uwajibikaji na uwazi wakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025.

Wizara ya Viwanda na Biashara, Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Viwanda, SLP 2996, 40478 Dodoma,
Tovuti: www.viwanda.go.tz